

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



Juni 07, 2023

TAARIFA KWA UMMA

RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. DKT. SAMIA SULUHU
HASSAN AMEWASALIMIA WANANCHI WA WILAYA YA LUDEWA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametangaza kuanza mara moja kwa mradi wa Liganga na Mchuchuma uliopo katika Mkoa wa Njombe Wilaya ya Ludewa mara baada ya kukamilika kwa zoezi la ulipaji wa fidia kwa Wanufaika 1142 waliopisha mradi huo.

Mhe. Rais Samia amesema hayo leo Juni 7, 2023 wakati akiongea na Wananchi wa Ludewa kwa njia ya simu kupitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka wakati wa uzinduzi wa zoezi hilo lililoongozwa na Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji.

Mhe. Rais Samia amesema, ***"Nilipopita kufanya kampeni nikiwa Makamu wa Rais niliahidi tutakuja kulipa fidia na mradi uanze, sasa leo ni furaha yangu kwamba timu ya Wataalumu wa Serikali ipo hapo Ludewa kwa ajili ya kulipa fidia, niwaahidi kwamba fidia zote zitalipwa na ahadi yetu baada ya kulipa fidia mradi sasa utaendelea, Mchuchuma na Liganga sasa unakwenda kuchangamka"***.

Kiasi cha shilingi Bilioni 15.4 kimeanza kulipwa kwa wanufaika wote wa Wilaya ya Ludewa ambapo Viongozi mbalimbali akiwemo Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka na Mbunge wa Jimbo la Ludewa Mhe. Joseph Kamonga wamemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali kwa niaba ya Wananchi.

A blue ink signature of Chrispin B. Kalinga.

Chrispin B. Kalinga

**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini (W)
LUDEWA.**

Ludewa ya Utalii, Uchumi wa Chuma na Makaa ya Mawe kwa Maendeleo Yetu.